

HUDUMA YA KWANZA NINI?

- Huduma ya kwanza ni ule usaidizi unao-
tolewa kwa haraka mara tu mtu anapopatwa
na ajali, jeraha ama anaposhikwa na
ugonjwa wa ghafla kabla kufikishwa hospi-
tali. Huduma hii inatolewa kwa kutumia vifaa
vilivyo karibu nasi.
- Zingatia: Huduma hii hutolewa kabla ya mje-
ruhiwa kupelekwa hospitali au kituo cha afya
kilicho karibu.

TUNATAMBUAJE MTOTO AKIWA MGONJWA?

- Joto kali.
- Kulia sana.
- Kukosa amani/kunyong'onyea/kukosa ucha-
ngamfu.
- Kukosa hamu ya kula au kunyonya.
- Kutetemeka mwili.
- Kutapika na kuhara.
- Kulala mara kwa mara pale inapotokea sio
kawaida ya mtoto.
- Kudidimia utosi, macho (kwa watoto wa-
changa).
- Kukauka mdomo.



MWANDAMO WA MWEZI UNA ATHARI YOYOTE KWA AFYA YA MTOTO?

- **HAPANA** - Hakuna uhusiano wowote kati ya
mabadiliko ya afya ya mtoto na mwandamo
wa mwezi. Haijathibitika kisayansi.



SHERIA KUU ZA KUTOA HUDUMA YA KWANZA?

- Fanya jambo la kwanza kwa haraka bila ku-
babaika.
- Mwendoe mgonjwa katika enao la ajali.
- Msaidie mgonjwa kupumua iwapo a-
nashindwa.
- Mfariji mgonjwa kwa ukaribu ili kumuondoa
wasiwasi.
- Usijaribu kupita kiasi.
- Usimvue mgonjwa nguo bila sababu, ila
legeza nguo zilizobana.
- Andaa kumpeleka hospitali kwa uchunguzi
wa tiba sahihi.



HOMA KWA WATOTO WADOGO

Tunatambuaje hali ya homa kwa mtoto?

- Homa ni pale joto linapokuwa juu zaidi ya
vile mama alivyomzoea mtoto wake. Katika
hali hii joto linakuwa zaidi kuliko kawaida
yaani zaidi ya nyuzi joto 37.
- Mara nyingi akina mama hugundua hali hii
kwa kupima watoto wao kwa kutumia
mikono nyuma ya kiganja.


Je huduma ya kwanza kwa mtoto mwenye homa ni ipi?

- Kumvalisha mtoto nguo nyepesi.
- Kumpa kinywaji baridi kinachopatikana (kisi-
cho na kilevi):
- Kumfariji mtoto ukimweleza kile unachom-
saidia kama vile kumpunguza nguo.

- Kuendelea kumlisha mtoto chakula kama kawaida yake:
- Kumpa mtoto dawa ya kutuliza maumivu (mfano Paracetamol) -kulingana na umri wa mtoto na uzito wake kama itakavyoagizwa na mtaalam. (angalia uzito kwenye kadi ya mtoto ya klinik).
- Mpeleke mtoto kituo cha afya au hospitali iliyo karibu na kueleza yote uliyoyafanya.

HALI ZA MARA KWA MARA ZINAZOWEZA KUHITAJI HUDUMA YA KWANZA

- Kuumwa/kung'atwa na wadudu, nyoka, wanyama, nyuki, nyigu, ng'e, siafu nk.
- Kuungua
- Kujikata (mfano wembe)
- Kuhara na Kutapika
- Chakula chenye sumu
- Mzio (allergy)
- Mafindofindo (tonsillitis)
- Kuumia jicho/macho
- Kupaliwa/kukwama na kitu



MAELEZO KWA AJILI YA MAWASILIANO

KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:

**KITUO CHA WATOTO YATIMA IRENTE
SIMU:**

**0754 844 777
0714 157 837**

MHUSIKA:



IRENTE CHILDREN'S HOME

© 2019 Prof. Dr. Ulrike Lütke,
Leibniz Universität Hannover
– All Rights Reserved –


ulrike.luedtke@ifs.uni-hannover.de



Niedersächsisches Ministerium
für Soziales, Gesundheit
und Gleichstellung

Kipeperushi hiki kimetengenezwa kwa msaada wa Wizara ya Ustawi wa Jamii, Afya na Fursa Sawa ya Jimbo la Lower Saxony, Ujerumani

MAFUNZO YA MALEZI YA AWALI NA MAKUZI YA MATAMSHI NA LUGHA KITUO CHA WATOTO YATIMA IRENTE, FEB 2018 - SEP 2019



HUDUMA YA KWANZA

Tunawashukuru washiriki wote wa Mafunzo kwa kutunga maudhui na kupigapicha mbalimbali zilizomo kwenye kipeperushi hiki.

Kwa sababu za kimaadili, tunadiriki kutoonyesha sura za watoto walioko kwenye picha.